Shirika la Kazi Duniani
Mpango wa Kimataifa unaohusu UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi

# Mwongozo wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) kuhusu UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi :

## Maswali na Majibu

### S. Kwa nini UKIMWI ni tatizo la mahali pa kazi?

J. UKIMWI ni tatizo la mahali pa kazi kwa sababu wengi wa waathirika ni wafanyakazi. UKIMWI huathiri ulimwengu wa kazi kwa njia mbalimbali: Hupunguza upatikanaji wa nguvu kazi pamoja na kupunguza kipato cha wafanyakazi wengi. Mahudhurio duni kazini huongeza gharama za ajira kwa waajiri. Pale wafanyakazi wanapoumwa wanalazimika kuacha kazi zao, na hivyo ujuzi na uzoefu wao hupotea. UKIMWI huathiri haki za msingi katika mahali pa kazi pamoja na kuathiri jitihada za kuwapatia wanawake na wanaume kazi zenye hadhi na kipato kizuri katika misingi ya usawa, uhuru, ulinzi na heshima. Waathirika wengi hawana msaada wa hifadhi ya jamii au wa matibabu. Ubaguzi dhidi ya watu wenye UKIMWI unaongeza hali ya kutokuwa na usawa katika jamii. UKIMWI huathari sana uchumi kwa sababu ya kushuka kwa tija, wakati ambapo idadi kubwa ya watoto yatima inayosababishwa na UKIMWI hupelekea watoto kujiingiza katika ajira wakiwa na umri mdogo. Kwa nchi zilizoathirika sana na mlipuko huo, maendeleo yaliyopatikana kwa miaka mingi yanahujumiwa. UKIMWI ni tishio kubwa kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

### S. Ni nini kimesababisha ILO kutayarisha Mwongozo huu kuhusu UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi?

J. Shirika la Kazi Duniani (ILO) limetayarisha Mwongozo huu kutokana na maombi mengi kutoka kwa washirika wake wakuu katika utatu ya kutaka ushauri kuhusu tatizo hili. Mwongozo huu unaonyesha juhudi za ILO kusaidia kuleta mazingira ya kazi yenye heshima na katika kukabiliana na tatizo hili kubwa kwa binadamu na maendeleo yake. Mwongozo huu ni sehemu muhimu ya mchango wa ILO katika juhudi za ulimwengu mzima za kupambana na janga la UKIMWI.

### S. Ni nini malengo ya mwongozo huu?

J. Madhumuni ya mwongozo huu ni kutoa maelekezo katika ulimwengu wa kazi na kusaidia kuzuia kuenea kwa maambukizo ya UKIMWI, na kupunguza athari zake. Mwongozo unatoa kanuni zinazopaswa kufuatwa na hatua muhimu ziweze kubuniwa katika mashirika, jumuiya na ngazi za kitaifa katika maeneo muhimu yafuatayo:

- kuzuia kuenea kwa UKIMWI
- kukabiliana na, na kupunguza athari za UKIMWI katika ulimwengu wa kazi
- kuwajali na kuwasaidia wafanyakazi walioathirika na walioambukizwa UKIMWI
- kuondoa hali ya kutowashutumu na kuwabagua watu ambao ni dhahiri kuwa wana UKIMWI au wanahisiwa kuwa na UKIMWI

Shirika la Kazi Duniani
Mpango wa Kimataifa unaohusu UKIMWI na Ulimwengu wa Kazi

## S. Kanuni za msingi za mwongozo huu ni zipi?

J. Mwongozo unazungumzia kanuni za msingi kama vile, kutowabagua watu ambao wana UKIMWI au watu wanaohisiwa kuwa wana UKIMWI katika ajira, usawa wa kijinsia, kupima na usiri, majadiliano ya jamii, kuzuia na kujali na kutoa msaada, kama misingi ya kuudhibiti mlipuko huo katika mahali pa kazi.

## S. Mwongozo huu ulianzaje?

J. Azimio la kuwa na mwongozo juu ya UKIMWI na ulimwengu wa kazi lilikubaliwa katika Mkutano wa Shirika la Kazi Duniani, mwezi Juni mwaka wa 2000, na kupelekea kuwa na programu maalum kuhusu UKIMWI katika Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani. Uamuzi wa Mkutano huo ulitaka kwamba miongozo ya kimataifa iandaliwe ili kudhibiti UKIMWI katika mahali pa kazi. Mwongozo huu ni matokeo ya ushirikiano kati ya ILO na sehemu zake tatu. Ulipitiwa upya na kuboreshwa zaidi na kikundi cha wataalam kutoka pande tatu na hatimaye kukubaliwa na Baraza Kuu la ILO, mwezi Juni mwaka wa 2001.

## S. Nani atautumia mwongozo huu?

J. Mwongozo unawahusu waajiri na wafanyakazi wote katika sekta za umma na sekta binafsi, na nyanja zote za kazi, zilizo rasmi na zisizo rasmi. Hii ni pamoja na serikali, waajiri na wafanyakazi na mashirika yao, watumishi wa huduma za afya katika mahali pa kazi, wataalam wa maswala ya UKIMWI, na wadau wengine wanaohusika. Mwongozo huu haukukusudiwa tu kwa nchi ambazo mlipuko huo una athari kubwa zaidi: malengo yake pia ni kuzuia kuongezeka kwa maambukizo kwa nchi ambazo hazijaathirika sana.

## S. Mwongozo huu utatumikaje?

J. Maelezo yaliyomo kwenye mwongozo huu yanazingatia sana kanuni na misingi ya ILO iliyokubalika, ambayo imetolewa kutokana na mazingira maalum ya mlipuko wa UKIMWI na athari zake katika ulimwengu wa kazi. Watengenezaji sera za kitaifa pamoja na washiriki katika mahali pa kazi wanaweza kuutumia kama msingi wa programu zao za kitaifa, sera za biashara au makampuni na makubaliano ya pamoja. Mwongozo huu unaweza kuwa chombo cha uhamasishaji, hasa kwa ajili ya kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kupigana vita dhidi ya UKIMWI, pamoja na kuwa mwongozo wa kuleta maendeleo na utekelezaji wa programu za mahali pa kazi na katika jumuiya.

## S. Ni nini kinafuata?

J.Mwongozo unaelezea umuhimu wa mahali pa kazi katika kujikinga na UKIMWI, kujali na kutoa msaada. Ulizinduliwa rasmi katika Mkutano Maalum wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kuhusu UKIMWI mjini New York, tarehe 25-27 Juni. Ijapokuwa ni chombo cha mwanzo, mwongozo wenyewe unaonyesha mwanzo tu. Changamoto kubwa inabakia katika uenezaji na utekelezaji wake na wadau wote husika. Mkurugenzi-mkuu wa ILO, Bw.Juan Somavia, amechukua hatua ya kuunda sera inayohusu UKIMWI kwa misingi ya mwongozo huu, na kuitumia katika shughuli za Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani. Atatoa wito kwa washiriki wote wa Mkutano Maalum-yakiwemo mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa-kuutumia mwongozo huu na kuhakikisha kwamba unafanyika utekelezaji wenye matokeo mazuri katika sehemu zao za kazi.

4, route des Morillons, CH-1211 Geneva 22, Switzerland, Website: www.oil.org Simu: (+41 22) 799 64 86, Fax: (+41 22) 799 63 49, Email: ILOAIDS@ilo.org
Kanda ya Africa Mashariki, S.L.P. 9212 Dar es Salaam, Tanzania. Simu: 255 22 21268821/4/6 Fax: 255 22 2126627 Email: daresalaam@ilo.org